**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA SABA

## KIKAO CHA KWANZA

**04 APRILI, 2017**

# OORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA SABA

## KIKAO CHA KWANZA – TAREHE 04 APRILI, 2017

**I. WIMBO WA TAIFA:**

**II. DUA KUSOMWA NA KIKAO KUANZA SAA TATU ASUBUHI:**

**III. KIAPO CHA UAMINIFU:**

Mhe. Salma Rashid Kikwete

**IV. TAARIFA YA SPIKA:**

**V. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

**1. MHESHIMIWA KHALIFA MOHAMED ISSA (MTAMBWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):- Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) upo katika Awamu ya Tatu ya utekelezaji wa mpango wa kunusuru

kaya maskini ili ziweze kumudu mahitaji ya chakula, elimu, afya na lishe bora kwa Watoto:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa ipo haja ya kuongeza viwango vya ulipaji kwa kaya maskini hasa ikizingatiwa upandaji wa bei za mahitaji ya kila siku na kuporomoka kwa thamani ya sarafu yetu;

(b) Je, ni vigezo gani vya uhakika vinatumika ili kupata kaya maskini.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**2. MHESHIMIWA AMINA SALEH MOLLEL (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Wakazi wanaoishi katika eneo la Hifadhi ya Ngorongoro wamekatazwa kulima kwenye maeneo wanayoishi kwa mujibu wa Sheria hali iliyochangia Wakazi wengi katika eneo hilo ambao ni Wafugaji kukabiliwa na njaa pamoja na umaskini mkubwa wa kipato:-

Je, ni lini Serikali itarekebisha Sheria ya Mamlaka ya Hifadhi, yaani "Ngorongoro Conservation Area Act, 1959 Revised Edition, 2002" ili Wananchi wa maeneo haya wapate maeneo kwa ajili ya shughuli zao za kilimo na ufugaji.

**WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:**

**3. MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE (BUNDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Zao la Pamba ndilo zao kuu katika Wilaya ya Bunda:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwapatia zao mbadala Wakulima wa zao la Pamba, baada ya zao hilo kuelekea kutokomea kutokana na matatizo ya bei ndogo isiyokidhi mahitaji ya uzalishaji wake;

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza uzalishaji wa zao la Pamba hasa ikizingatiwa kuwa Wilaya ya Bunda yenye Majimbo matatu inategemea viwanda vya Pamba katika mapato na ajira.

**4. MHESHIMIWA LEAH JEREMIAH KOMANYA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi:- Serikali imeweka kipaumbele kwenye Sekta ya Kilimo na kuainisha kwamba mazao ya Kilimo yatakuwa moja ya malighafi kwenye viwanda nchini:-

(a) Je, Serikali imeweka mkazo gani kwenye vyanzo vya kilimo ambavyo ndivyo vitakuwa malighafi na kusababisha uzalishaji ukue;

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa uhakika utakaowezesha Wakulima wengi zaidi kuingia kwenye kilimo cha umwagiliaji;

(c) Je, Serikali imewekeza kwa kiasi gani kwenye zana za kilimo za kisasa kwa Wakulima wadogowadogo hasa wanawake waishio Vijijini.

**WIZARA YA NISHATI NA MADINI:**

**5. MHESHIMIWA IGNAS ALOYCE MALOCHA (KWELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Serikali ilituthibitishia kuwa gesi aina ya Hellium iligundulika katika Ziwa Rukwa na kwamba gesi hiyo ina thamani kubwa na ni adimu sana Duniani:-

Je, ni lini Serikali itaanza kuchimba gesi hiyo ili Watanzania waanze kunufaika nayo kabla haijagunduliwa au kuchimbwa mahali pengine Duniani.

## WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

### 6. MHESHIMIWA KASUKU SAMSON BILAGO (BUYUNGU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Kwa muda wa miaka 9 sasa baadhi ya Wananchi wa Wilaya ya Kakonko nyumba zao zimewekwa "X" kwa lengo la kuvunjwa ili kupisha ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami:-

(a) Je, ni Wananchi wangapi kati ya hao wenye alama ya "X" kwenye nyumba zao wanakidhi vigezo vya kulipwa na sababu ni zipi kwa wasiolipwa;

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kitatumika kulipa fidia za nyumba hizo;

(c) Je, fidia hiyo itazingatia gharama ya nyumba kwa sasa au gharama ya zamani ya nyumba zilipowekwa "X" na ni lini watalipwa.

7. **MHESHIMIWA JOYCE BITA SOKOMBI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Barabara ya kutoka Tarime kwenda Serengeti ni barabara muhimu sana kwa Wakazi wa Wilaya hizo na kwa maisha yao ya kila siku:-

Je, ni lini barabara hiyo itajengwa kwa kiwango cha lami.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

8. **MHESHIMIWA BHANGWANJI MAGANLAL MEISURIA (CHWAKA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Inapotokea wazazi wametengana na Mama akaondoka na mtoto na kwenda kuishi naye; lakini tangu wazazi hao watengane Mama hatoi nafasi kwa Baba kwenda kumtembelea mtoto:-

Je, Baba ataipata wapi haki hiyo ya kumuona mtoto.

9. **MHESHIMIWA ANNE KILANGO MALECELA (KUTEULIWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Ndoa za utotoni kwa sasa zimekithiri sana na ndoa hizi zina athari kubwa ndani ya Jamii:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutokomeza ndoa hizi za utotoni.

**DODOMA**
**04 APRILI, 2017**

**DKT. T. D. KASHILILAH**
**KATIBU WA BUNGE**